

# **MALUMBANO**

# **BAINA YA**

# **SUNNI NA SHIA**

**Kimeandikwa na:**  
Sheikh Abdilahi Nassir

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**

**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN: 978-9987-427-50-5**

**Kimeandikwa na:**

**Sheikh Abdilahi Nassir**

**Ahlul Bayt Centre**

S. L. P. 84603, Mombasa, Kenya

**Simu:** +254 41 311515

**Mobile:** +254 733 705425

**E-mail:** ahlulbaytcentre@yahoo.com

**Chapa ya kwanza:** 2004

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**

Al-Itrah Foundation

**Chapa ya pili:** Januari, 2008

**Nakala:** 2000

**Chapa ya tatu:** Novemba, 2017

**Nakala:** 1000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**

Al-Itrah Foundation

P. O. Box 19701, Dar-es-Salaam, Tanzania

**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555

**Baruwa Pepe:** alitrah@yahoo.com

**Tovuti:** [www.ibn-tv.com](http://www.ibn-tv.com)

**Vitabu mtandaoni:** [www.alitrah.info/ebooks/](http://www.alitrah.info/ebooks/)

---

# **YALIYOMO**

---

Neno La Mchapishaji .....	2
Malumbano .....	6
Kwa nini Shia tafauti na Sunni .....	6
Kwa nini Maimamu 12?.....	7
Mtume (s.a.w.w.) amesema tuwafuate hao .....	15
Ushahidi wa hilo .....	18
Ahlul Bayt si wake wa Mtume (s.a.w.w) .....	22
Maimamu 12 ndio Ahlul Bayt.....	25
Imam Mahdi a.f.....	26
Khitilafu kati ya Maimamu wa Kisunni.....	27
Khitilafu za Makhalifa wa Kisunni.....	32
Khitilafu za masunni wao kwa wao .....	33

Masunni wazozana na kutukanana.....	35
Masunni wakufurishana .....	36
Amri ya kufuata makhalifa na majibu yake .....	40
Kuswalisha si huja .....	43
Hakukuwa na Ijmaa (komangano) .....	50
Imam Ali (a.s) hakunyamaza bali aligomba .....	55

## SHUKURANI

Shukrani nyingi kwa Baraza la ilimu ya Kiislamu (The Islamic Education Board of the World Federation of Khoja Shia Ithna Asheri Muslim Communities) la London, Uingereza kwa kugharimia uchapaji wa kitabu hiki. Mwenyezi Mungu awalipe malipo mema, amin

## SHUKURANI

Tunamshukuru Sheikh Abdilahi Nassir kwa kuturuhusu sisi Al-Itrah Foundation kuchapisha kitabu chake hiki **“Malumbano Bainya ya Sunni na Shia”** toleo la tatu nakala 1000.

Ni matumaini yetu kwamba wasomaji wetu watanufaika na mtiririko huu wa malumbano baina ya Sunni na Shia. Huu sio ugomvi ni kuulizana maswali na kujibiana. Tunamshukuru sana Sheikh kwa kuandika kitabu hiki. Tunamuombea kila la kheri, Allah *Aza wa Jalah* ampe tawfiq azidi kutuelimisha kwa kalamu yake ya maarifa na upole.

**Al-Itrah Foundation  
Dar es Salaam**



---

## NENO LA MCHAPISHAJI

---

**K**itabu kilichoko mikononi mwako ni kitabu kili-choandikwa kwa lugha ya Kiswahili na Sheikh Abdilahi Nassir kwa jina la “**Malumbano Bainan Sunnah wal-Shia**”,

Kitabu hiki, “**Malumbano Bainan Sunnah wal-Shia**” ni matokea ya khutba zake nyingi zenyenye kuelimisha, nyingi zikuwa kwenye kanda za kaseti na CD, mihad-hara, darasa zake na tafakari ya muda mrefu.

Malumbano sio ugomvi (wanavyoweza kutafsiri watu wengine) bali ni kuulizana maswali na kujibizana kwa njia ya kistaarabu, hoja, elimu na akili. Na hivi ndivyo alivyofanya Sheikh wetu huyu kwa kuandika kitabu hiki kwa mtindo wa maswali na majibu, ili kumfanya msomaji aelewé upande ule una maswali gani na upande huu una majibu gani kuhusu maswali hayo. Na kama alivyoeleza Sheikh katika utangulizi wake kwamba njia hii huenda ikamsaidia Shia anapokabiliwa na

maswali kama haya, bali pia itamsaidia Sunni kuelewa sababu za Mashia kuamini wanayoamini. Na sisi tuko pamoja na Sheikh katika hili.

Kutokana na ukweli huo, sisi wahudumu wenu wa Taasisi ya ‘Al-Itrah Foundation’ tukaamua kumuomba Sheikh tutoe toleo la pili kwa kitabu hiki kwa toleo la kwanza limekwisha na halipo kwenye mzunguko, na watu wengi wanakiulizia kitabu hiki.

Basi alihamdu’li-llahi hili ni toleo la pili. Tunamshukuru Sheikh wetu kwa kutukubalia kuchapisha toleo hili na tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa toleo hili.

Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni mwanga kwa wasomaji wetu na kuzidisha upeo wao wa elimu ya dini.

### **Al-Itrah Foundation**

الْيَسِيرُ الْحَلِيمُ

---

# MALUMBANO

---

## KWA NINI SHIA NI TAFAUTI NA SUNNI

**SUNNI:** Nyinyi Shia, kwa nini mambo yenu mengi ni tafauti na yetu sisi, Sunni, ambao ndio wengi kuliko wafuasi wa madhihabi yote mengine?

**SHIA:** *Kwanza;* yataka uelewe kwamba wanaojiita Shia si kundi moja; ni makundi mengi. Mimi, kwa hivyo, siwezi kuyasemea makundi yote hayo. Niwezalo kulisemea mimi ni kundi la Shia Ithnaashari.

*Pili;* yataka uelewe vile kwamba hata nyinyi Sunni hamuko kundi moja. Muko madhihabi mane yenye khitilafu zenu vile vile baina yenu. Madhihabi hayo ni yale ya Hanafi, Maaliki, Shaafi, na Hambali.

*Tatu;* yataka uelewe vile kwamba wingi si hujja. Kuwa Sunni ndio wengi kuliko madhihabi mengine si alama ya kuwa wao ndio wenye haki. Bali uki-soma Qur’ani Tukufu (Sura 6:116) utaona inakwambia kwamba “ukiwafuata wengi wa walio duniani wataku-poteza na njia ya Mwenyezi Mungu”! Na ukitaka kuelawa zaidi kwamba wingi si hujja soma, kwa mfano,

Sura 2:243; 5:49 na 103; 6:111; 7:187; 10:92; 11:17; 16:83; 17:89; 21:24 na 26:223.

**SUNNI:** Hata hivyo, kwa nini ziweko tafauti baina yenu na sisi ilhali sote tunamuamini Mwenyezi Mungu Mmoja na Mtume Muhammad s.a.w.w., tunakubali kuwa Qur'ani ndicho Kitabu Chake, na tunaposwali tunalekeea kibla kimoja, na mengi mengine? Kwa nini?

**SHIA:** Ni kwa sababu sisi, baada ya Bwana Mtume s.a.w.w., tunafuata uwongozi wa maimamu 12, ambao wote ni kizazi chake, katika mambo yote hali nyinyi mwawafuata maimamu wane katika masiala ya kifikihi, na mmoja katika masiala ya akida (imani). Kwa kuwa yanayofundishwa na maimamu wetu na wenu yanatafautiana, ndipo sisi tukakhitalifiana.

## KWA NINI MAIMAMU 12?

**SUNNI:** Na kwa nini nyinyi mukawafuata hao maimamu wenu 12, musiwafuate hawa wetu watano?

**SHIA:** Tunawafuata hawa wetu 12 kwa sababu hivyo ndivyo alivyotuagizia Mtume Muhammad s.a.w.w. kabla ya kuaga dunia. Yeye hakutuagizia tuwafuate hao wenu watano!

Mbali na hivyo, kati ya hao watano, wane *wao wenye* wamekataa kufuatwa katika kila walilolisema. Wamewambia watu watizame; lolote walilolisema, lilio kinyume na la Mtume s.a.w.w., waliache.

**SUNNI:** Wamesema wapi hayo?

**SHIA:** Tuanze na Imam Shaafi' i, mwenye wafuasi wengi kuliko wote huku Afrika ya Mashariki. Yeye, kwa mfano, amesema: "Mukipata, katika kitabu changu, kilicho kinyume na sunna ya Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w.w., basi semeni yaliyosemwa na sunna ya Mtume wa Mwenyezi Mungu na *acheni niliyoyasema mimi*." Hayo, mionganini mwa vitabu vyengine, utayapata katika uk 361 wa Juzuuy ya Pili ya *I'laamul Muuqi'iin* ya Ibnu'l Qayyim al Jawzii.

Vile vile amesema: "Niliyoyasema, na ikawa Mtume s.a.w.w. amesema kinyume na niliyoyasema, basi lililoswihi katika Hadith ya Mtume ni bora (ku-fuatwa), *wala musinifuate mimi*." Hayo pia unaweza kuyaona katika uk 285 wa Juzuuy ya Pili ya hicho hicho kitabu tulichokitaja hapo juu, mionganini mwa vyengine.

Imam Abuu Haniifa naye, ambaye ndiye wa pili baada ya Imam Shaafi' i mwenye wafuasi wengi huku Afrika ya Mashariki, amesema: "Maneno yangu haya ni rai (yangu), nayo ndiyo bora niliyoweza kuipata.

Basi yoyote atakayetujia na neno zuri zaidi kuliko letu, huyo ni bora zaidi kuswibu kuliko sisi.” Hayo utaya-pata katika uk 75 wa Juzuuy ya Kwanza ya hiyo hiyo *I'laamul Muuqi'iin*.

Vile vile alipoulizwa: “Ewe Abuu Haniifa! Haya unayoyafutu ndiyo haki isiyo na shaka?” Alijibu: “Sijui, *hwenda ikawa ni batili isiyo na shaka...*”!

Pia inasimuliwa na mmoja wa wanafunzi wake kuwa: “Tulikuwa tukenda kwa Abuu Haniifa pamoja na Abuu Yusuf na Muhammad bin Hasan. Tukawa tu-naandika (kila) anachosema. Siku moja akamwambia Abuu Yusuf: “Ee wee! *Usiandike kila unachokisikia kwangu*. Hwenda nikawa na rai moja leo, kesho nikaicha; na nikawa na rai (nyengine) kesho, kesho kutwa nikaicha...” Maneno haya yamenukuliwa na Abuu Zahra katika kitabu chake kiitwacho *Abuu Haniifa*.

Wa tatu mwenye wafuasi wengi huku kwetu, siku hizi, ni Imam Ahmad bin Hambal. Yeye, kama ili-vyo katika uk 211 wa Juzuuy ya Pili ya hiyo *I'laamul Muuqi'iin*, amesema “*Usinifuate mimi!* Wala usimfuate Maalik! Wala Shaafi'i! Wala Awzaa'i! Wala Thawrii! Bali chukueni walipochukuwa wao.”

Vile vile amesema: “Rai ya Awzaa'i na rai ya Maalik, na rai ya Abuu Haniifa – zote ni rai, na zote zi sawa

kwangu. *Kwa hakika hujja ni iliyomo katika Hadith.*” Hayo nayo utayapata katika uk 79 wa Juzuuy ya Kwanza ya *I'laamul Muuqi'iin*.

Imam wane ni Maalik ambaye hana wafuasi wengi huku kwetu. Yeye, kwa mujibu wa uk 211 wa Juzuuy ya Ishirini ya *Fataawaa Ibni Taymiyya*, amesema: “Hakika mimi ni binadamu. Hukosea na hupata. Basi itizameni rai yangu. Kila ambayo imewafikiana na Qur'an na Sunna, ichukueni. *Na kila ambayo haikuwafikiana na Qur'an na Sunna, iachen'i.*”

Ukiyazingatia maneno ya maimamu wenu hayo - na hapa nimeacha kuyanukuu ya vitabu chungu nzima vyengine - itakudhihirikia kwamba walikuwa wakati mwengine wakisema maneno kwa rai zao tu. Maneno kama hayo ndiyo waliyokataza watu kuyafuata, kama yatakwenda kinyume na ya Bwana Mtume s.a.w.w. Hivyo ni sawa na kusema kuwa walisema maneno kwa maoni (jitihadi) yao tu ambayo hawakuwa na hakika nayo kuwa ndivyo alivyotaka Bwana Mtume s.a.w.w. Kwa ajili hii ndiyo sisi tukakataa kuwafuata wao.

**SUNNI:** Sasa turejee kwa hao wenu 12. Mtume s.a.w.w. ameagizia wapi tuwafuate wao?

**SHIA:** Maagizo hayo utayaona hata katika vitabu vyenu vya Hadith munavyovikubali na kuvienzi, kama *Sahih Bukhari* na *Sahih Muslim!*

**SUNNI:** Jee! Unaweza kunitajia Hadith hizo zilipo katika vitabu hivyo, na zinavyosema?

**SHIA:** Ndiyo! Katika *Sahih Bukhari*, ambacho kwenu nyinyi ndicho kitabu sahihi mno baada ya Qur'ani Tukufu, Hadith hizo zimo katika kitabu cha *Al-Ahkaam*, Mlango wa *Sayakuumuthnay Ashara Amiiraa* (kwa Kiarabu). Kwa tafsiri ya Kiingereza ya kitabu hicho hicho, utazipata katika Juzuuy ya 9, uk 250, Hadith Na. 329. Nayo yasema hivi: “Jaabir b. Samura amesema: Nilimsikia Mtume s.a.w.w. akisema: *Kutakuwa na maamiri* (watawala) *kumi na wawili*. Akasema maneno ambayo sikuyasikia vizuri. Babangu akasema: Yeye amesema: *Wote* (watawala hao) *watakuwa ni makureshi*”

Na katika *Sahih Muslim*, ambacho kwenu nyinyi ndicho kitabu kilicho sahihi mno baada ya *Sahih Bukhari*, utazipata Hadith hizo (kwa Kiarabu) katika kitabu cha *Al-Imara*, Mlango wa *An-Nasu Taba'ul Liqurayshi*. Kwa tafsiri ya Kiingereza ni Hadith Na. 4477, 4478, 4480-83 zilizomo katika uk 1009-11 wa Juzuuy ya 3 ya kitabu hicho. Nazo zasema hivi:

*Hadith Na. 4477:* Jaabir b. Samura amesema, ‘Nilingia kwa Mtume s.a.w.w. mimi na babangu, nikamsikia akisema: *Huu Ukhilifa hautakwisha mpaka kuptikane makhalifa kumi na mbili mionganini mwao*. Kisha

akasema maneno yaliyonifichikia. Nikamuuliza babangu: Amesemaje? Akanijibu (kuwa amesema): *Wote watakuwa ni makureshi.*"

*Hadith Na. 4478:* "Jaabir b. Samura amesema, 'Nimemsikia Mtume s.a.w.w. akisema: *Mambo ya watu hayataacha kuendelea vizuri mpaka watawaliwe na watu kumi na mbili.* Kisha Mtume s.a.w.w. akasema maneno yaliyonifichikia. Nikamuuliza babangu: Amesemaje Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w.w.? Akanijibu (kuwa amesema): *Wote watakuwa ni makureshi.*

*Hadith Na. 4480:* "Jaabir b. Samura amesema, 'Nimemsikia Mtume s.a.w.w. akisema: *Uislamu hau-taacha kuwa na nguvu mpaka kuwe na makhalifa kumi na mbili.* Kisha akasema maneno ambayo sikuyafahamu. Nikamuuliza babangu: Amesemaje? Akanijibu (kuwa amesema): *Wote watakuwa ni makureshi.*"

*Hadith Na. 4481:* "Jaabir b. Samura amesema, 'Mtume s.a.w.w. amesema: *Dini hii haitaacha kuwa na nguvu mpaka kuwe na makhalifa kumi na mbili.* Kisha akasema kitu ambacho sikukifahamu. Nikamuuliza babangu: Amesemaje? Akanijibu kuwa amesema: *Wote watakuwa ni makureshi.*"

*Hadith Na. 4482:* "Jaabir b. Samura amesema, 'Nilikuwa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w.w., mimi

na babangu, nikamsikia akisema: *Dini hii haitaacha kuwa na nguvu na kutawala mpaka kuwe na makhalifa kumi na mbili.* Akasema maneno ambayo sikuyasikia kwa kelele za watu. Nikamuuliza babangu: Amesemaje? Akanijibu (kuwa amesema): *Wote watakuwa ni makureshi.*”

*Hadith Na. 4483:* “Aamur b. Said b. Abii Waqqaas amesema: Nilimwandikia barua Jaabir b. Samura ni kampa kijana changu, Naafi’i, (ampelekee) ili anieleze kitu alichokisikia kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w.w. Akaniandikia, ‘Nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w.w., siku ya Ijumaa jioni, alipopigwa mawe Aslami mpaka akafa (kwa kuzini), akisema: *Dini (hii) haitaacha kuendelea mpaka Kiyama kisimame au mutawaliwe na makhalifa kumi na mbili, wote wakiwa ni makureshi...*”

**SUNNI:** Lakini katika Hadith hizo tunaambiwa tu kuwa viongozi hao ni 12, na kwamba wote watakuwa makureshi. Hazitwambii tuwafuate!

**SHIA:** *Kwanza;* ni haba kwamba mimi nimekutajia idadi ya 12 ambayo ndiyo idadi ya maimamu wetu tynaofuata uwongozi wao? Jee! Wewe unaweza kunitajia angalau Hadith moja tu inayowaagiza nyinyi kufuata hao maimamu wenu 4 au 5? Kama wewe huwezi, tafad-

hali wa ulize mashekhe wako wakupatie ili uniletee na mimi niione. Anwani yangu utaiyona mwanzo mwanzo wa kitabu hiki.

*Pili;* ni kweli kwamba, kwa Hadith zilizotajwa katika vitabu viwili hivyo tulivyovitaja hapo juu, ni vigumu kuelewa kwamba hawa tunaowafuata sisi ndio hao. Lakini kitu kimoja kinaweza kutusaidia. Nacho ni hiki cha kuwa wote watakuwa makureshi.

Kwa kuwa hawa tunaowafuata sisi, wote ni wa ukoo wa Mtume Muhammad s.a.w.w.; na kwa kuwa yeye ali-kuwa Kureshi, ni wazi kwamba na wao ni makureshi. Kwa hivyo kwa hili wameitimiza bishara iliyomo katika Hadith hizo.

Hapa inataka uelewe kwamba, kati ya madhihabi yote ya Kiislamu, hakuna madhihabi hata mamoja yanayofuata maimamu 12 ambao *wote* ni makureshi isipokuwa sisi. Na hiyo ndiyo sababu ya kuitwa Shia Ithnaashari, kutokana na neno la Kiarabu *ithnaashara* ambalo maana yake ni *kumi na mbili*.

Hata hivyo, kama kwa Hadith tulizozitaja hapo juu hatuoni amri yoyote ya kuwafuata, katika Hadith nyengine za Bwana Mtume s.a.w.w. amri hiyo imeta-jwa. Na hilo li wazi kwa yoyote anayesoma vitabu vy-enu!

**SUNNI:** Jee! Unaweza kunitajia Hadith hizo na zilipo?

### **MTUME S.A.W.W. AMESEMA TUWAFUATE HAO**

**SHIA:** Naam, naweza. Wala kwa sasa sitakutajia zote maana ni nydingi. Nitakutajia kidogo tu ambazo zitatosha kujibia suali yako.

*Ya kwanza ni ile Hadith ijulikanayo kwa jina la “vizito viwili” (thaqalayni). Nayo yasema hivi: “Enyi watu! Mimi nawaachia nyinyi vitu viwili ambavyo, kama mutavifuata, hamutapotea kabisa: Kitabu cha Mwenyezi Mungu na ahlu bayt wangu.”*

Maneno hayo, katika vitabu vyenu vya Hadith, yamesimuliwa kwa riwaya mbalimbali - zote zikiwa na lengo moja tu: la kutuusia tufuate vitu viwili hivyo, baada ya Bwana Mtume s.a.w.w. kufariki dunia, ili tusipotee. Waliozisimulia riwaya hizo ni maswahaba wasiopungua.30! Pia tumeelezwa kwamba Bwana Mtume s.a.w.w., ili kutuonyesha umuhimu wa agizo hili, ameyarudia maneno hayo mahali mbalimbali, k.v. Madina: juu ya mimbari ya msikiti wake, Arafa katika Khutba ya Kuagana, Ghadir Khum, na katika khutba yake baada ya kuondoka Twaif.

Kwa maneno “kama mutavifuata, hamutapotea kabisa” ni wazi kwamba Bwana Mtume s.a.w.w. alitaka tuvifuate vyote vitu viwili alivyovitaja katika Hadith yake hiyo. Kwa maneno mengine ni kwamba, kama mtu atakifuata kimoja na kukiacha cha pili, bila shaka atapotea. Hili li wazi zaidi tunapoizingatia ile riwaya ya Twabaraani isemayo: “Musiwatangulie, wala musibaki nyuma nao maana mutaangamia; wala musi-jaribu kuwafundisha maana wao wanajua zaidi kuliko nyinyi.”

Hadith *ya pili* ni ile isemayo: “Tambua! Hakika mfano wa *ahlu bayt* wangu kwenu ni kama safina ya Nuhu; yoyote aliyeipanda aliokoka, na yoyote aliye-baki nyuma nayo alighariki.”

Kuelewa jinsi watu wa Nabii Nuhu walivyoghariki, soma Sura 11:36-49. Hivyo, kama watu wa Mtume huyo walivyoghariki baharini kwa kutopanda safina yake, asemavyo Bwana Mtume Muhammad s.a.w.w., ndivyo watakavyoghariki wafuasi wa Mtume Muhammad s.a.w.w. kwa kutowafuata *ahlu bayt* wake. Hapa duniani watakuwa wameaswi, na kesho Akhera wataadhidiwi!

Hadith *ya tatu* ni ile isemayo: “Nyota huwahifadhi wakazi wa duniani wasighariki, na *ahlu bayt* wangu hu-

wahifadhi umma wangu wasikhitalifiana ( katika mambo ya duniani ). Kwa hivyo kabilia yoyote ya Waarabu itakapowakhali (itakapowapinga) *ahlu bayt* wangu (katika hukumu za Mwenyezi Mungu) basi nayo itakhitilifiana iwe chama cha Iblis.”

Kwa Hadith hii Bwana Mtume s.a.w.w. anatuhakikishia kwamba, kama tutafuata *ahlu bayt* wake, tutakuwa na msimamo mmoja katika mambo yetu ya dini; hatutakhitalifiana. Lakini kama tutayapuuza mafunzo yao, na kwenda kinyume nayo, bila shaka tutakuwa na khitilafu baina yetu, tuwe kama chama cha Iblis (Shetwani).

Na hilo li wazi unapolinganisha msimamo wa maimamu wetu kumi na mbili na misimamo ya maimamu wenu katika mambo ya dini. Wetu wana msimamo mmoja; hawakukhitalifiana. Wenu wana misimamo mbalimbali; wamekhitalifiana. Kwa kuwa sisi tunawafuata maimamu walio na msimamo mmoja, hatukukhitalifiana. Lakini kwa kuwa nyinyi munawafuata maimamu waliokhitalifiana, nanyi pia mumekhitalifiana mpaka mukaweza hata kukufurishana!

**SUNNI:** Kabla hatujaendelea mbele, mimi hapa nina suali tano kwa haya uliyoyasema sasa hivi:

- i. Umenitajia Hadith tu; hukunitajia umezitoa katika vitabu gani vyetu. Jee! Unaweza kunitajia tafadhali?
- ii. Unaweza kunitajia majina ya hao “maswahaba wasiopungua 30” usemao kwamba wameisimulia Hadith hiyo kwa riwaya mbalimbali?
- iii. Katika Hadith ulizozitaja hapo juu, naona unachukulia ahlu bayt wa Mtume s.a.w.w. kuwa ndio hao maimamu wenu kumi na mbili, hali ninavyoilewa mimi ni wake wa Mtume s.a.w.w. Ama sivyo?
- iv. Maimamu wetu wamekhitalifiana katika mambo gani ya dini?
- v. Sisi nasi tumekhitalifiana wapi hata tukakufurishana?

## USHAHIDI WA HILO

**SHIA:** Ahsanta. Suali zako nitazijibu japo kwa ufupi. Tuanze na *suali ya kwanza*.

Majina ya vitabu ambamo waweza kuzipata Hadith hizo ni mengi sana. Lakini hapa chini nitakutajia majina machache tu.

*Hadith ya kwanza*, kwa riwaya mbalimbali, utaipata katika vitabu vifuatavyo:

*Musnad Ahmad*: Jz 3, uk 17 na 26; na Jz 5, uk 182 na 189. *Mustadrak ya Haakim*: Jz 3, uk 109, 148 na 533. *Sunan Tirmidhi*: Jz 5, uk 328, Hadith 3874; na uk 329, Hadith 3876. *Kanzul Ummaal*: Jz 1, uk 154, Hadith 873; na uk 165, Hadith 945. *Majma'uz Zawaaid*: Jz 9, uk 162 na 163.

*Al-Jaami'us Swaghiir*: Jz 1, uk 353.

*Jaami'ul Usuul ya Ibnul Athiir*: Jz 1, uk 187, Hadith 65 na 66. *Mishkaatul Maswaabiih*: Jz 3, uk 258.

*Maswaabiihus Sunnah ya Baghawi*: Jz 2, uk 279. *Usudul Ghaabah ya Ibnul Athiir*: Jz 2, uk 12.

*Al-Mu'jamus Swaghiir ya Twabaraani*: Jz 1, uk 135.

(l) *Al-Mu'jamul Kabiir ya Twabaraani*: uk 137.

*Hadith ya pili* utaipata katika vitabu vifuatavyo:

(a) *Mustadrak ya Haakim*: Jz 2, uk 343 na Jz 3, uk 150.

(b) *Musnad Ahmad*: Jz 5, uk 92. *Muntakhab Kanzil Ummaal* iliyoko pembezoni mwa *Musnad Ahmad*: Jz 5, uk 95. *Majma'uz Zawaaid ya Haythamii*: Jz 9, uk 168. *Al-Mu'jamus Swaghiir ya Twabaraani*: Jz 1, uk 139; na

Jz 2, uk 22. *Al-Jaami'us Swaghiir* ya Suyuutwii: Jz 2, uk 132. *As-Swawaa'iqul Muhriqah* ya Ibn Hajar: uk 184 na 234.

*Hadith ya tatu* utaipata katika vitabu vifuatavyo: *Mustadrak* ya Haakim: Jz 2, uk 448; na Jz 3, uk 457.

*Muntakhab Kanzil Ummaal* iliyoko pembezoni mwa *Musnad*

*Ahmad*: Jz 5, uk 93. *Majma'uz Zawaaid*: Jz 9, uk 174. *Al-Jaami'us Swaghiir*: Jz 2, uk 161. *As-Swawaa'iqul Muhriqah*: uk 150 na 234.

**SUNNI:** Jee! Hao maswahaba? Ni nani na nani?

**SHIA:** Kati ya maswahaba waliosimulia Hadith ya “vizito viwili” ni hawa wafuatao:

1. Alii b. Abii Twaalib
2. Hasan b. Alii b. Abii Twaalib
3. Fatma bt. Muhammad s.a.w.w.
4. Salmaan Al-Faarisi
5. Abuu Dharr al-Ghifaari
6. Ibn Abbas
7. Abuu Said al-Khudri

8. Jaabir b. Abdillaahi al-Ansaaarii
9. Abdul Haytham b. at-Tiihaan
10. Abuu Raafi'
11. Hudhayfa b. al-Yamaan
12. Hudhayfa b. Asyad al-Ghifaarii
13. Khuzayma b. Thaabit Dhush Shahaadatayni
14. Zayd b. Thaabit
15. Zayd b. Arqam
16. Abuu Hurayra
17. Abdulla b. Hantwab
18. Jubayr b. Mut'am
19. Al-Barraa' b. Aazib
20. Anas b. Maalik
21. Twalha b. Abdillaahi at-Taymii
22. Abdulrahman b. Awf
23. Sa'd b. Abii Waqqaas
24. Amru b. al-Aas
25. Sahl b. Sa'd al-Ansaaarii

26. Adiy b. Haatim
27. Abuu Ayyuub al-Answaarii
28. Abuu Shurayh al-Khuzaa'ii
29. Uqba b. Aamir
30. Abuu Qudaama al-Answaarii
31. Abuu Layla al-Answaarii
32. Dhwamiira al-Aslamii
33. Aamir b. Layla b. Dhumra
34. Ummu Salama, mke wa Mtume s.a.w.w.
35. Ummu Haani', dada wa Imam Alii a.s.

### AHLUL BAYT SI WAKE WA MTUME S.A.W.W.

**SUNNI:** *Ahlul bayt si wake wa Mtume s.a.w.w.? Sivyo isemavyo Sura 33:33?*

**SHIA:** Hivyo ndivyo munavyosema nyinyi, lakini sisi hatusemi hivyo kwa sababu zifuatazo:

- i. Kama wake wa Bwana Mtume s.a.w.w. ndio *ahlul bayt* waliotajwa katika Sura 33:33, bila shaka aya hiyo - kulingana na nahau (sarufi) ya Kiarabu - isingeandikwa hivyo. Ingeandikwa

kwa kutumia dhamiri ya wanawake, si ya wanaume kama ilivyo katika aya hiyo. Kwa maelezo zaidi ya hili, tizama uk 52-56 wa tafsiri yetu ya Sura al-Ahzaab.

- ii. Ni jambo lijulikanalo na wasomi wote wa Kiislamu kwamba iliposhuka aya hiyo, Bwana Mtume s.a.w.w. alichukua guo (kishali) akajifinika yeje pamoja na Imam Alii, Bibi Fatma, Hasan na Husein; kisha akasema: “Hawa ndio *ahlu bayt* wangu...” Hilo ni kuonyesha kwamba alivyoielewa Mtume s.a.w.w. aya hiyo sivyo walivyoielewa mashekhe wenu! Jee, utamfuata nani hapo?
- iii. Wasomi wote wa Kiislamu wanajua kwamba, walipojifinika hilo guo, Bibi Ummu Salama - mmoja wa wake wa Mtume - alitaka kuingia humo. Lakini Bwana Mtume alimzuiya; hakumruhusu! Jee, hapo Bwana Mtume hakujua kwamba wake zake ndio *ahlul bayt*? Mbona alimzuiya mke wake huyo kuingia guoni?
- iv. Hata Bibi Aisha, ambaye ni mmoja wa wake za Mtume s.a.w.w., amelitambua hilo; kwamba Ahlul Bayt katika aya hiyo, ni wale

waliofinikwa guo na Bwana Mtume s.a.w.w. Tiz. Sahih Muslim, “Kitaabul Fadhaail”, Mlango wa “Fadhaailu Ahlil Bayt.” Kwa Kiingereza ni Jz 4, uk 1293-1294, Hadith 5955.

- v. Yeye mwenyewe Bwana Mtume s.a.w.w., alipokuwa akenda msikitini kuswali alfajiri, alikuwa akipita nyumba ya Bibi Fatma a.s. huku akilingana “Swalaal! Swalaal! enyi ahlul bayt !” Kisha akisoma aya hiyo uliyoitaja wewe. Kwa nini kupita kwa Bibi Fatma a.s. tu, aliko Imam Alii na watoto wake a.s., asiwapitie wake zake, kama kweli *ahlul bayt* ni wake wa Mtume s.a.w.w.?

Hizo ndizo sababu zetu za kukatalia kuwa *ahlul bayt* ni wake wa Mtume s.a.w.w. Zaidi ya hayo, katika hiyo hiyo Sura ya 33 (*al-Ahzaab*) na kabla ya hiyo aya ya 33, Mwenyezi Mungu amewataja wake wa Mtume s.a.w.w. mara sabaa. Mara tano amewataja kwa jina la *az'waaj* (tiz. aya ya 6, 28, 50, 53, 59), na mara mbili (tiz. aya ya 30 na 32) amewataja kwa *nisaan-nabiyy*. Mbona hakuwataja kwa *ahlul bayt*?

**SUNNI:** Lakini hapa pana mushkili! Upande mmoja wasema *ahlul bayt* ni hao waliotajwa kuifafanulia aya

niliyokutajia hapo juu, ambao ni watu watano. Upande wa pili wasema ni hao maimamu wenu 12! Sasa, tushike lipi hapo? Watano au kumi na mbili?

## MAIMAMU 12 NDIO AHLUL BAYT

**SHIA:** Shika yote mawili kwa sababu ndivyo alivyosema Bwana Mtume s.a.w.w. Katika Hadith ya vizito viwili, tuliyokwisha kuiyona hapo nyuma, kati ya hao maimamu 12, waliofinikwa guo ni watatu tu: Imam Alii na wanawe wawili -Hasan na Husein a.s. Hao wengine tisia hawakuwahi kufinikwa kwa sababu walikuwa bado hawajazaliwa.

Lakini, kabla ya kuaga dunia, Bwana Mtume s.a.w.w., kama tulivyoonyeshana mwanzo huko nyuma (uk 7-8), alitwambia - kama twataka tusipotee - tushikamane na vitu viwili. Kimoja ni Qur'ani Tukufu. Cha pili ni *ahlul bayt* “wangu”. Kisha akaongeza kwamba “viwili hivyo havitatengana mpaka vije vikutane” naye huko Akhera. Kwa hivyo, kama tutasema kwamba *ahlu bayt* ni hao watatu tu, itakuwa na maana kwamba, kuanzia mwaka wa 61H alipofariki dunia Imam Husein a.s., Qur'ani imebaki peke yake; haina mwenzake! Na hilo ni muhali kwa sababu litabatilisha kauli ya Bwana Mtume s.a.w.w. ambaye “hatamki neno kwa kutamani ye

tu, isipokuwa huwa ni wahyi alioteremshiwa na Mwenezezi Mungu.”(Sura 53:3-4). Sasa? Lililobaki ni tutizame kama kuna mahali popote ambapo Bwana Mtume s.a.w.w. ametutatulia utata huu. Na hilo tutaliona kwa zile Hadith zake tulizotangulia kutajiana humu (uk 4-6), za kuwa wote watakuwa 12, kuwa ndizo zinazowiana na Hadith ya vizito viwili. Vyenginevyo, haviwi.

**SUNNI:** Lakini sasa, hata hao maimamu wenu 12 si washakufa wote? Kwa hivyo, tangu alipokufa wa mwisho wao, si Qur’ani “imebaki peke yake; haina mwenziwe”? Utalielezaje hilo?

### **IMAM MAHDI A.F**

**SHIA:** Kwa imani yetu, kumi na moja tu kati ya hao ndio waliokufa. Huyo wa 12 aliyezaliwa mwaka wa 255H, angali hai mpaka leo. Ndiye ye ye atakayetokea kama Imam Mahdi kabla ya Kiyama.

**SUNNI:** Yaani, kwa huu mwaka tulionao leo wa 1423H, umri wake ni miaka 1168?! Na anaishi wapi?

**SHIA:** Hilo nakuomba tuliache kwa sasa, maana lina-taka kikao chake peke yake. Inshallah tutakapomaliza haya tulivoanza nayo, tutalijadili na hilo. Kwa sasa tuendelee na hizo suali zako ambazo hijazimaliza.

**SUNNI:** Heewallwa! Suali yangu ya (iv) ni kukhusu maimamu wetu wane; wao wamekhitalifiana katika mambo gani ya dini?

### **KHITILAFU KATI YA MAIMAMU WA KISUNNI**

**SHIA:** *Kwanza* napenda ujue kwamba maimamu wenu hawakuwa ni wane! Walikuwa zaidi ya hao; lakini kwa sababu za kisiasa, ambazo hapa si mahali pake kuzzungumza, hao wengine wamezama!

**Pili**, hao wane hawakuishi wakati mmoja; waliishi nyakati mbalimbali. Abuu Haniifa, kwa mfano, alizaliwa mwaka wa 80H, akafa mwaka wa 150H. Imam Maalik alizaliwa mwaka wa 93H, akafa mwaka wa 179H. Imam Shaafi'i alizaliwa mwaka wa 150H, akafa mwaka wa 204H. Na Imam Hambali alizaliwa mwaka wa 164H, akafa mwaka wa 241H.

Sasa, ukizitizama tarehe zao hizo, na ule mwaka aliofia Mtume s.a.w.w. (10H), itakudhihirikia kuwa *maimamu hao hawakuonana na Mtume kamwe*. Imam Abuu Haniifa alizaliwa miaka 70 baada ya kufa Mtume s.a.w.w.; Imam Maalik, miaka 83; Imam Shaafi'i, miaka 140; na Imam Hambali, miaka 154.

**Tatu**, kwa maimamu wane hao, nyinyi hamuchukui dini yote. Munachukua masiala ya kifikihi tu. Masiala

ya kiimani (aqida), munayachukua kwa Abul Hasan al-Ash'ari; ndiyo sababu mukaitwa ma-Ash'arii vile vile. Imam wenu huyu alizaliwa mwaka wa 260H, miaka 250 baada ya kufa Mtume s.a.w.w., na kuaga dunia mwaka wa 333H.

**SUNNI:** Ni kweli maimamu wetu hawakuna-na na Bwana Mtume s.a.w.w. Lakini walionana na *mataabi'ina* (waandamizi) walioonana na maswahaba ambao ndio kiungo chetu na Bwana Mtume s.a.w.w. Jee, hilo halitoshi?

**SHIA:** Hapo ndipo pia palipo na tafauti ya nyinyi na sisi. Nyinyi munaamini kuwa maswahaba wote ni waadilifu; hawatiliki makosa. Kwa hivyo munalikubali kila lililonasibishwa na wao na waandamizi wao.

Sisi hatuamini hivyo; hatuamini kuwa *wote* wali-kuwa waadilifu. Tunaloamini ni kuwa *baadhi yao* wa-likuwa waadilifu. Lakini baadhi nyengine hawakuwa hivyo. Walikuwa wauwaji, walevi, wazinifu, waongo, na kadhaalika. Hao hatuwaamini.

Hata hivyo, maswahaba hao pia hawakuwa na kauli moja. Mara nyingi walikhitalifiana katika riwaya zao za waliyoyapokea kwa Bwana Mtume s.a.w.w. , na katika hukumu za sharia walizozitoa wao. Khitilafu hizi zilipokewa na waandamizi (*taabi'ina*) wao waliopokea

kwao; na wao nao wakawarithisha maimamu wenu waliopokea kwao. Ndipo na nyinyi nanyi - wafuasi wa maimamu hao - mukawa na khitilafu hizi mulizonazo zilizowafikisha hadi ya kupigana na kukufurishana nyinyi kwa nyinyi.

**SUNNI:** Lakini si maimamu wetu peke yao ambaو ha-wakukutana na Mtume Muhammad s.a.w.w. Hata wenu pia ni vivyo hivyo! Unasemaje juu ya hilo?

**SHIA:** Ni kweli, lakini *sio wote*. Watatu wa kwanza - Alii, Hasan na Husein a.s. - walimwona. Waliobakia walipokezana yale waliyoyasikia kwa waliowatangulia ambaو hawakuwa wanafunzi wa yoyote nje ya silsila (*chain*) yao. Kwa ajili hii ndiyo imam wetu wa sita, Imam Ja'far as-Swaadiq a.s., akasema kuwa maneno aliyyotwambia yeye aliyasikia kwa babake, na babake aliyasikia kwa babu yake, (vivyo hivyo mpaka) na babu yake aliyasikia kwa Imam Alii a.s. ambaye naye aliyasikia kwa Mtume s.a.w.w., aliyeypokea kwa Jibriil a.s., aliyeypokea kwa Mwe-nyezi Mungu s.w.t. Na hii ndiyo inayoitwa *silsilatudh dhahabiyya* (mnyororo wa dhahabu). Haina mshawasha.

Tukikumbuka kwamba Mtume s.a.w.w., katika Hadith yake maarufu, amesema kwamba yeye ni “jiji la il-

imu” na Imam Alii a.s. ni “lango lake”; na tukikumbuka kwamba maimamu wote waliokuja baada ya Imam Alii a.s. waliipata ilimu yao kwake, tutaweza kuelewa kwa nini maimamu wetu hawakukhitalifiana wao kwa wao kama walivyokhitalifiana maimamu wenu, japokuwa baadhi yao vile vile hawakumwona Mtume s.a.w.w.

**SUNNI:** Sasa nieleze; maimamu wetu wamekhitalifiana katika mambo gani ya dini?

**SHIA:** Wamekhitalifiana katika mambo mengi. Hapa, kwa sababu ya dhiki ya nafasi, sitakudondolea yote. Nitakuteulia machache tu.

Kwa mfano, kutokwa na manii hakutangui (hakuvunji) udhu kwa Shaafi’i. Lakini kwa Hanafi, Maaliki na Hambali kunatangua.

Mfano mwengine ni wa udhu. Kwa Shaafi’i na Hambali ni lazima kuufuanisha (*tartiib*); yaani uanzie uso, mikono, kichwa na mwisho miguu. Lakini kwa Hanafi na Maaliki, si lazima. Unaweza kuanzia miguu na kumalizia uso; yaani kinyumentyume.

Mfano wa tatu ni wa swala ya maiti. Kwa Shaafi’i na Hambali, husoma sura ya *alhamdu* baada ya takbir ya kwanza. Lakini kwa Maaliki na Hanafi haisomwi.

Mfano wane ni wa takbira ya swala ya Idd. Kwa Hanafi, baada ya *takbiiratul ihraam* (kufunga swala), hupiga takbira *tatu*. Kwa Shaafi'i ni *sabaa*. Kwa Hambali na Maaliki ni *sita*. Katika rakaa ya pili, Hanafi hupiga takbira *tatu*; lakini Shaafi'i na Hambali na Maaliki hupiga *tano*.

Tukija kwenye najisi; twaona kuwa mbwa *si* najisi kwa Maaliki. Lakini kwa Hanafi, Shaafi'i na Hambali *ni* najisi. Hali kadhaalika manii ya binadamu; kwa Maaliki na Hanafi *ni* najisi. Lakini kwa Shaafi'i na Hambali *si* najisi; ni tohara.

Mwisho tuingie kwenye ndoa. Jee mtu aweza kumuowa bintimwanaharamu wake? Shaafi'i na Maaliki wasema *aweza*; ni halali. Lakini Hanafi na Hambali wasema *hawezo*; ni haramu.

Nataraji mifano michache hii inatosha kuthubutishia hujja yetu.

**SUNNI:** Lakini wewe wawalinganisha maimamu wetu wa fikihi na maimamu wenu wa uwongozi wa dola kwa jumla. Na hiyo si sawa! Sawa ni uwalinganishe hao na makhalifa wetu k.v. Sayyidna Abubakar na Sayyidna Umar. Jee hao pia walikhitalifiana?

## KHITILAFU ZA MAKHALIFA WA KISUNNI

**SHIA:** Ndiyo! Hata wao pia hawakuwa na hukumu moja katika lilo hilo jambo moja. Kwa mfano, kukhusu wanawake wa wale Waislamu “walioritadi” katika Ukhalifa wa Abubakar, alipowashika mateka katika Vita vya Ridda, Abubakar aliwafanya watumwa (wajakazi)! Lakini Umar, aliposhika Ukhalifa, aliitangua hukumu hiyo. Badali yake, aliwarudisha kwa watu wao wakiwa huru, isipokuwa wale waliozaa na bwana zao. Mionganoni mwa hao ni Khawla binti Ja’far al-Hanafiyya, mamake Muhammad bin Alii bin Abii Twaalib.

Kukhusu ardhi walizoziteka; Abubakar aliwagawanya wale walioshiriki katika vita. Umar, wakati wake, alikataa kufanya hivyo. Badali yake, alizifanya wakfu; hakuzigawanya!

Kukhusu ruzuku za mali ya umma; Abubakar aliwagawanya watu kwa usawa. Umar hakufanya hivyo! Badali yake, aliwafadhilisha baadhi juu ya baadhi.

Pia kumbuka! Umar hakumteuwa mtu maalumu kuwa Khalifa baada yake. Lakini Abubakar aliteuwa! Alimteuwa yeeye Umar!

Kuna na mengine ambayo hapana haja ya kuyataja. Nadhani hayo mane yatakutosha kwa leo.

**SUNNI:** Sisi nasi tumekhitalifiana wapi hata tukakufurishana?

### **KHITILAFU ZA MASUNNI WAO KWA WAO**

**SHIA:** Kwa kufuata maimamu waliokhitalifiana, nyinyi nanyi pia mumekhitalifiana na kufika hadi ya kuzozana, kukufurishana na hata kuuwana! Hayo si ya kale tu, bali yangaliko hadi hii leo; humu humu mwetu Afrika ya Mashariki.

Ukitaka kuziona khitilafu zenu, mbali zile chache tulizozitaja za maimamu wenu, ingia msikiti wowote wenu uangalie jinsi watu wanavyoswali. Wengine utawaona wamefunga mikono; wengine hawakuifunga, bali wameinyosha. Wale walioifunga pia wamekhitalifiana! Wengine wameifungia juu ya kitovu. Wengine chini ya kifua. Wengine juu ya titi (ziwa) la kushoto; na wengine chini ya shingo kamwe!

Tujapo kwenye kikao cha *tahiyyaatu (tashahhud)*, utaona wengine -wafikapo kwenye shahada - hawaki-inui kidole chao cha shahada. Wengine hukiinua. Wale wanaokiinua, wengine hukinyosha tu na kukituliza. Wengine hukitikisa juu na chini. Wengine hukitikisa kulia na kushoto, na wengine hukizungusha kama wa-naochora harufi ya O!

Tukija baada ya *samiallahu liman hamida*, wengine husujudu moja kwa moja. Wengine la! Kwanza hurudi wakafunga mikono yao kama ilivyokuwa kabla ya *samiallahu*, kisha ndipo wakasujudu!

Tumeona khitilafu zenu katika swala ya Idd (uk 19). Vivyo hivyo mumekhitalifiana katika swala ya tarawehe. Wengine mwaswali rakaa 20; wengine 8! Katika swala ya alfajiri; wengine mwakunuti, wengine hamukunuti.

Sasa katika sampuli zote hizo, ni sampuli ipi khaswa aliyoiswali Bwana Mtume s.a.w.w.? Au ni sampuli zote?

Tukumbuke kwamba Bwana Mtume s.a.w.w., katika Hadith yake mashuhuri, ametwambia: “Swalini kama mulivyoniona mimi nikiswali.”

Tukumbuke pia kwamba hakuwa akiswali swala zake kwa siri. Popote alipokuwa yeze, yeze ndiye aliye kuwa imamu. Kwa hivyo maswahaba walikimwona anavyoswali. Vile vile tukumbuke kwamba maswahaba, kwa mapenzi waliyokuwa nayo ya Mtume Muhammad s.a.w.w., walikuwa wakilihifadhi kila walilomwona akilifanya - hata alivyokuwa akenda njiani, alivyokuwa akizungumza na kucheka, alivyokuwa akilala, alivyokuwa akila, alivyokuwa akipiga msuwaki

na kuchana nywele zake, na kadhaalika. Na yote hayo yamesimuliwa na kuhifadhiwa katika vitabu vya Hadith na sera. Basi kama wameweza kutuhifadhia yote hayo, na kama hayo - ambayo si ya faradhi - wameshindwa kutuhifadhia jinsi alivyokuwa akiswali: jambo ambalo ni la faradhi? Mbona hakuna kauli moja katika hili?

## **MASUNNI WAZOZANA NA KUTUKANANA**

**SUNNI:** Tumezozana wapi na kutukanana?

**SHIA:** Kwanza, mumezozana katika swala ya tarawehe. Kabla ya madhhabi mapya kuja, yaliyozuka katika hizi zama zetu huko Saudi Arabia, nyote mulikuwa mukiswali tarawehe rakaa 20. Mukaambiwa sivyo! Ni rakaa 8. Mukazozana na kushambuliana madarasani mpaka misikiti yenu ikagawanyika - baina ya ile iswaliyo rakaa 20, na ile ya rakaa 8. Ikawa wa huku haswali kule, na wa kule haswali huku!

Hali ikawa vivyo hivyo kukhusu swala ya alfajiri. Zamani mulikuwa mukikunuti. Mulipoambiwa haifai, mukagawanyika na kushambuliana madarasani. Zogo likaenea mpaka mabarazani. Misikiti nayo ikagawanyika - baina ya inayokunuti na isiyokunuti. Muliokuwa mukiswali msikiti mmoja mukawa mwaswali misikiti mbalimbali; munaokunuti hamswali kusikokunutiwa,

na musiokunuti hamswali kunakokunutiwa - hata kuwe karibu nanyi!

Mbali vurugu la mwezi wa Ramadhani na Idd. Ni nani asiyelijua hilo?

**SUNNI:** Jee, kukufurishana na kuuwana; tume-fanyiana wapi na lini hayo?

### **MASUNNI WAKUFURISHANA**

**SHIA:** Tuanze na kukufurishana.

Kama kawaida yangu, sitakuchokesha kwa mifano mingi. Nitakutajia michache tu.

Wa kwanza ni ule wa Sheikh Muhammad b. Musa. Huyu alikuwa ni Hanafi na kadhi wa Dimishq (*Damascus*); alifariki mwaka wa 506H. Yeye alisema: “Lau mimi ningekuwa na amri yoyote, ningewatoza *jizya* ma-Shaafi’i.”

Wa pili ni ule wa Sheikh Abuu Haamid at-Tuusii aliyefariki mwaka wa 567H. Yeye naye alisema: “Lau mimi ningekuwa na amri, ningewatoza *jizya* Hambali.”

Kwa faida yako na wasomaji wetu, inataka uelewe kwamba *jizya* ni aina ya kodi ambayo dola ya Kiislamu huwatoza makafiri. Kwa hivyo Mwislamu anapotamani

kuwatoza *jizya* Waislamu wenzake, huwa tayari amewafanya sawa na makafiri!

Mfano wa tatu ni wa Sheikh Abuu Haatim. Huyu alikuwa Hambali na alisema, “Yoyote ambaye si Hambali, basi si Mwislamu!” Kwa maneno mengine, Waislamu wote ni makafiri isipokuwa wao Hambali!

Mfano wane ni wa Sheikh Ibn Taymiyya aliyefariki mwaka wa 728H. Huyu ndiye ambaye fikra zake zili-kuja zikafuatwa na kukuzwa na Sheikh Muhammad b. Abdulwahhaab, mwanzilishi wa madhhabiy ya Wahabi; naye alikuwa ni Hambali. Kwa fikra zake na misimamo yake iliyokuwa tafauti na ya Waislamu wengine, Waislamu wa madhhabiy yasiyokuwa yake walikomanga-na na kutangaza, Dimishq na miji mengine, kwamba “Yoyote anayefuata dini ya Ibn Taymiyya, mali yake na damu yake ni halali.” Kwa maneno mengine, wao ni makafiri wa kutendewa wanayotendewa makafiri!

Wa tano ni wa Sheikh Alii b. Hasan, aliyekijulikana pia kwa lakabu ya Saifuddiin, ambaye alifariki mwaka wa 631H. Yeye kwanza alikuwa Hambali. Kisha akawa Shaafi’i. Wanazuoni wenziwe wakamfanyia chuki na kumuhukumu kuwa ni “kafiri na mzandiki”!

Hayo ni ya karne nyingi zilizopita. Hebu tuangalie ya huu wakati wetu; yenu nyinyi na mawahabi, ambao

hujifanya ni masunni wenzenu, popote wanapotaka muwasaidie katika chuki zao dhidi yetu sisi mashia. Kweli wao, kama nyinyi hamuyakubali madhhibabi yao, wanawakubali kuwa mu Waislamu? Hasha! Nyinyi kwao mu makafiri kama walivyo makafiri wowe; mali yenu, hishima yenu, na damu yenu ni halali kwao!

Kwa maneno ya Sheikh Hamad b. Nasir b. Uthman an-Najdii, aliyekuwa mmoja wa wanafunzi wa Sheikh Muhammad b. Abdulwahhaab, na ambaye alifariki mwaka wa 1225H, “Mtu yoyote anayesema hakuna mungu ila Mwenyezi Mungu, na Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, lakini akaendelea na ushirikina wake wa kuwalingana maiti na kuwaomba wamkidhie haja zake na kumfariji mazito yake, basi *huyo ni kafiri na mushrik ambaye damu yake na mali yake ni halali hata kama asema hakuna mungu ila Mwenyezi Mungu, na Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na (hata kama) aswali na kufunga na adai kuwa yeye ni Mwislamu.*” Kwa maneno mengine, masunni wengi ambaio si shirki kwenu kuomba mawalii na watu wema, kwa mawahabi nyinyi si makafiri tu, bali ni halali kuwauwa na kuyateka nyara mali yenu - hata kama mwawali na kufunga!

Japokuwa maneno haya yalisemwa na shekhe huyo mwaka wa 1211H, yaani miaka 212 iliyopita, lakini mpaka leo hiyo ingali imani ya wafuasi wa shekhe huyo ( mawahabi) ambao huwambia nyinyi ni masunni wenzao kwa *taqiyya* tu! Kwa sasa wanaficha kucha zao kwa sababu hawajakuwa na sirikali yao ya kuwaweza-sha kufanya hivyo. Mara tu watakapojiona wana uwezo huo, hawatasita kuitekeleza imani yao hiyo- ya kuuwa na kupokonya Waislamu mali yao - kama walivyofanya huko Mashariki ya Kati waliposhirikiana Mfalme Ibn Su'ud na Sheikh Muhammad b. Abdulwahhaab kuisimamisha dola ya Kiwahabi. Waliuwa maelfu kwa maelfu ya masunni na mashia na kuwapokonya mali yao.

Huku kwetu Afrika ya Mashariki, kwa kujijua kwamba hawajawa na nguvu za kidola, hawajajasiri kuweta nyinyi makafiri wala kuwapokonya mali yenu. Waliloweza kulifanya mpaka sasa hivi, ni kuweta wale kati yenu musiokubali madhihabi yao, mushrikina(!) huku wakiendelea kujifanya ni ndugu zenu mpaka wakati wao utakapowadia. Ushahidi wa hili ni yale yaliyowapata mwaka jana (2001 B.K.) huku Mombasa na Nairobi. Kwa kujiona sasa wana nguvu, kwa ajili wafuasi wao wanazidi kuongezeka, walilivunja lile kaburi lililokuwa Msikiti wa Sheikh Jundani, Mombasa,

na lile lililokuwa Msikiti wa Imtiyaaz, Nairobi. Lau kama musingesimama kidete, bila shaka wangeyavunja makaburi mengine yote ya mawalii wenu na kuifukua mifupa yao kama walivyofanya lile la Sheikh Jundani.

**SUNNI:** Hebu sasa tuache haya ya zama zetu; turejee zama za Mtume Muhammad s.a.w.w. Kutilia nguvu imani yenu juu ya maimamu wenu kumi na mbili, ulinitajia Hadith za Mtume s.a.w.w. Kisha ukaribia kwamba, kama na sisi tunao ushahidi wa maneno yake, unaotilia nguvu imani yetu juu ya makhalifa wetu, nikutajie (uk 6-7).

**SHIA:** Ndiyo; nilikwambia kweli hivyo. Kwani unao?

### **AMRI YA KUFUATA MAKHALIFA NA MAJIBU YAKE**

**SUNNI:** Naam; ninao. Na wangu ni ushahidi wa aina tatu: wa aya za Qur'ani Tukufu; wa kitendo chake mwenyewe Bwana Mtume s.a.w.w.; na wa mmojawapo wa misingi ya sharia ya Kiislamu. Jee, wapenda nianzie wapi?

**SHIA:** Anzia ushahidi wa hizo aya za Qur'ani Tukufu.

**SUNNI:** Vyema! Katika Qur'ani Tukufu, Mwenezezi Mungu anasema (Sura 42:38): "Na mambo yao

(huyafanya kwa) kushauriana.” Vile vile anamwambia Mtume wake s.a.w.w. (Sura 3:159): “Na shauriana nao katika mambo.”

**SHIA:** Sasa ndiyo umekusudia kusema nini hapo?

**SUNNI:** Nililokusudia kusema, kama wanavyosema wanazuoni wetu, ni kuwa makhalifa wawekwe kwa kushauriana; na kwamba hata yeye mwenyewe, Bwana Mtume, aliamrishwa ashauriane na swahaba zake.

**SHIA:** Naam; hivyo ndivyo nyinyi munavyozieleza aya hizi. Lakini hivyo sivyo asilan. Sisi hatuyakubali maelezo yenu hayo kwa sababu zifuatazo:

**Kwanza;** zote aya mbili hizo hazikhusiani kabisa na Ukhilifa wala Uimamu. Ukweli ni kwamba hiyo aya ya kwanza (Sura 42:38) inakhusiana na mambo ambayo Mwenyezi Mungu na Mtume wake hawajayatolea hukumu. Hayo ndiyo mambo ambayo maswahaba waliruhusiwa kushauriana. Lakini yale ambayo Mwenyezi Mungu na Mtume Wake walikuwa washayatolea uamuzi, Qur’ani inatueleza wazi (Sura 33:36) kwamba Waislamu hawakuwa tena na kхиari nayo; hawakuwa na uwezo wa kushauriana juu ya hayo. Na hili la uwongozi wa Waislamu baada ya Bwana Mtume s.a.w.w. (Ukhilifa au Uimamu) ni kati ya mambo yaliyokwisha kuamuliwa na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake,

kama tulivyokwisha kuona huko nyuma (uk 4-9). Basi vipi litaamuliwa tena na maswahaba kwa kushauriana? Maswahaba wanao uwezo wa kubatilisha lililoamuliwa na Mwenyezi Mungu na Mtume Wake s.a.w.w?

**Pili;** kama kwa aya hiyo, Mwenyezi Mungu alitaka maswahaba washauriane kukhusu Ukhalfifa, mbona Abubakar (Khalifa wa Kwanza) hakufanya hivyo? Pale alipomteuwa Umar awe Khalifa wa Pili, na akaandika waswia iwe hivyo, mbona hakushauriana na maswahaba wenziwe? Basi, kwa kitendo chake hicho, si ameaswi amri ya Mwenyezi Mungu?

**Tatu:** kukhusu hiyo aya ya pili uliyoitaja (Sura 3:159) ya Mwenyezi Mungu kumwamrisha Mtume s.a.w.w. ashauriane na maswahaba wake. Kama, munavyodai nyinyi, Mwenyezi Mungu alimuamrisha Mtume Wake s.a.w.w. ashauriane na maswahaba wake kukhusu Ukhalfifa, itabidi tukiri kuwa Bwana Mtume s.a.w.w. - Mwenyezi Mungu apishe mbali-alimuaswi Mwenyezi Mungu kwa sababu hakuna kumbukumbu yoyote tuliyochiwa kwamba Bwana Mtume s.a.w.w. alilifanya hilo! Jee, inawezekana Bwana Mtume s.a.w.w. kumuaswi Mwenyezi Mungu? Bila shaka haiwezekani. Kwa hivyo tumbakiwa na suali nyengine. Nayo ni: Alipoamrishwa ashauriane na mas-

wahaba wake, ilikuwa ni katika mambo gani kama si kukhusu Ukhilifa?

Hilo tutalielewa vizuri tunapotambua kuwa hiyo aya uliyoitaja wewe (ya Sura 3:159) imekuja kati ya aya ya 139 na 166 ya sura hiyo. Sasa, tunapozisoma aya hizo tunaona wazi kuwa zinazungumzia mambo ya vita. Kwa hivyo aliloamrishwa Mtume s.a.w.w. hapo ni ashauriane na maswahaba wake katika mambo ya vita; na hilo, kwa mujibu wa kumbukumbu za kihistoria zilizoko, alilifanya. Hata hivyo, kutokana na aya hiyo hiyo ya 159, uamuzi wa mwisho - baada ya kushauriana nao - aliachiwa yeye Mtume s.a.w.w. *peke yake.*

Hizo ndizo sababu zetu za kukatalia maelezo yenu ya aya ulizozitaja kukhusu kuchaguliwa Khalifa kwa kushauriana.

## KUSWALISHA SI HUJJA

**SUNNI:** Jee hujja ya kuswalisha; hicho si kitendo cha Bwana Mtume s.a.w.w., yeye mwenyewe? Si yeye aliyemteuwa Sayyidna Abubakar awaswalishe watu pale yeye alipokuwa mgonjwa mpaka akatawafu? Huo si ushahidi tosha wa Mtume s.a.w.w. kutaka Sayyidna Abubakar awe Khalifa wake baada ya yeye kuondoka duniani?

**SHIA:** Kwetu sisi, na hata kwenu nyinyi, ushahidi huo hauna mashiko kwa sababu zifuatazo:

**Kwanza;** kwenu nyinyi, kuswalisha si chochote! Kama ni chochote musingelimwachia mtu yoyote kuswalisha - “awe mwema au muovu”, kama mudaivyo kuwa Bwana Mtume s.a.w.w. amesema hivyo! Kama mtu muovu aweza kuwa imamu wa kuswalisha watu, pana shani gani ya Khalifa Abubakar kuteuliwa kuswalisha watu?

**SUNNI:** Kabla hujaendelea mbele, Bwana Mtume s.a.w.w. amesema wapi kuwa mwema na muovu aweza kuwa imamu?

**SHIA:** Kwa mujibu wa vitabu vyenu, Mtume s.a.w.w. amesema: “Swalini nyuma ya kila mwema (*barrin*) na muovu (*faajir*)”. Hadith hiyo ni mashuhuri kwenu. Na ukiitaka, kati ya vitabu uwezamo kuipata ni *Kanzul Ummaal*, uk 54 wa Juzuu ya Sita (Hadith Na. 14815). Na hilo linaonekana kila siku misikitini mwenu. Kama mumechelewa mathalan, baada ya swala ya jamaa kubwa, si dasturi yenu kufunga swala nyuma ya yoyote munayemkuta anaswali - muwe munamjua au hamum-jui, ajua au hajui, ni mwema au ni muovu?

**Pili;** Hadith za Bwana Mtume s.a.w.w. kumuachia Khalifa Abubakar kuswalisha watu zina utata mwin-

gi; bali zinapingana zoo zenyewe kwa zenyewe! Kwa hivyo hatuwezi kuzitegemea.

**SUNNI:** Utata huo ni upi, na Hadith hizo ziko wapi?

**SHIA:** Kwa mfano, kuna inayosema kuwa aliposwali nyuma ya Abubakar Bwana Mtume s.a.w.w. alikuwako mkono wake wa kushoto. Kuna inayosema kuwa ali-kuwako mkono wake wa kulia. Kuna inayosema kuwa alikuwa nyuma yake. Sasa, tushike lipi hapo? Zote hizo unaweza kuziona katika uk 367-368 na uk 384 wa Juzuu ya Kwanza ya *Sahih Bukhari* ya Kiingereza (Hadith Na. 651 na 681).<sup>1</sup>

**Tatu;** kwa mujibu wa riwaya zenu, Bwana Mtume s.a.w.w alikwenda msikitini na Abubakar yumo katika swala. Mtume naye akaingia katika swala hiyo. Ndiyo au siyo?

**SUNNI:** Ndiyo!

**SHIA:** Ikiwa ni hivyo basi, lazima iwe ni mojawapo ya mambo matatu. Ama Mtume s.a.w.w. ndiye ali-yejikuwa imamu wa swala hiyo, na Abubakar na wengineo wakawa maamuma. Au Abubakar ndiye aliyejikuwa imamu, na Mtume s.a.w.w. na wengineo wakawa maamuma! Au Bwana Mtume s.a.w.w. na Abubakar, wao wawili pamoja, walikuwa maimamu na wengineo wakawa maamuma. Sawa?

**SUNNI:** Sawa.

**SHIA:** Kama ni hilo la kwanza, la Mtume kuwa ndiye aliyekuwa imamu, na Abubakar akawa maamuma, basi nyinyi hamutakuwa tena na hujja. Maana itakuwa Abubakar siye aliyeswalisha! Aliyeswalisha ni mwe-nyewe Bwana Mtume s.a.w.w.

Kama ni hilo la pili, la Abubakar kuwa ndiye aliyekuwa imamu na Mtume s.a.w.w. akawa maamuma, itabidi tukubali kuwa Bwana Mtume s.a.w.w. alijiuzulu uimamu wake akajitenga na Utume wake. Maana kama Mwenyezi Mungu amewakataza Waislamu wasimtangulie Mtume Wake (Sura 49:1), vipi ye ye atamtanguliza Abubakar katika swala asiwe amevunja amri ya Mola wake? Na kama Mwenyezi Mungu amewakataza Waislamu wasiinue sauti zao mbele ya Mtume Wake (Sura 49:2), vipi ye ye atamwacha Abubakar ainue sauti yake katika swala, na yeye yupo? Si itakuwa vile vile amevunja amri ya Mola wake? Jee, Mtume s.a.w.w. aweza kufanya hivyo? Hasha! Hawezi. Wala hakuna Mwislamu anayeweza kusema kuwa anaweza.

Kama ni hilo la tatu, la Bwana Mtume s.a.w.w. na Abubakar – wote wawili pamoja – kuwa maimamu wa swala moja, bila shaka litakuwa ni kioja! Tangu

lini swala moja ikawa na maimamu wawili? Hilo halikuswihi kwenu wala kwetu.

Sasa tuendelee na sababu zetu nyengine za kukatalia maelezo yenu ya kwamba, kwa kumteuwa Abubakar kuswalisha, Bwana Mtume s.a.w.w. alikusudia kumfanya yeye ni Khalifa wake baada yake.

Sababu yetu ya *nne* ni hii: ni kwamba wanahistoria wamekomangana kwamba Bwana Mtume s.a.w.w. alimpeleka Abubakar katika jeshi la Usaama bin Zayd kwenda kupigana na Warumi. Basi vipi Abubakar mmoja huyo atakuwa katika jeshi la Usaama *nje ya Madina*, na wakati huo huo aweko *ndani ya Madina* anaswalisha watu? Haiwezekani!

Sababu yetu ya *tano* inatokana na riwaya ya Bibi Aisha, binti yake yeye Khalifa Abubakar. Katika uk 13 wa Juzuuy ya Tano ya *Sahih Bukhari* ya Kiingereza<sup>2</sup> (Hadith Na. 19), Bibi Aisha anaeleza kuwa, alipokufa Bwana Mtume s.a.w.w., Abubakar hakuwako Madina! Alikuwako mahali paitwapo Sunhu, kiasi cha kilomita 5 hivi kutoka Madina. Kwa hivyo ni wazi kwamba, siku hiyo aliyatawafu Bwana Mtume s.a.w.w., yeye hakuswali swala yoyote ya mchana ndani ya Madina. Basi vipi itakuwa kwamba Mtume s.a.w.w. alimuamrisha yeye aswalishe watu?

Sababu yetu ya *sita* ni kwamba, hata kama tutakubali kuwa Bwana Mtume s.a.w.w. alimteuwa Abubakar kuswalisha, hilo pekee halimfanyi yeze kuwa Khalifa wa Mtume s.a.w.w. baada yake. Maana, kama ni hivyo, basi Abdulrahman bin Awf naye ingelazimu awe Khalifa kwa sababu, kama inavyoiezwa na Ibn Kathiir katika uk 22 wa Juzu ya Tano ya kitabu chake, *Al Bidaaya Wan Nihaaya*, Mtume wa Mwenyezi Mungu s.a.w.w. aliswali jamaa nyuma yake! Kama hilo halikumfanya yeze kuwa Khalifa, kwa nini limfanye Abubakar?

Hali kadhaalika Amru bin al-Aas; Bwana Mtume s.a.w.w. alimteuwa kuwa amiri wa Abubakar na Umar, na *muhaajiriin* wengine na *answaar* katika vita vya *Dhaatus Salaasil*. Na, kwa mujibu wa Ibn Kathiir (uk 273 wa Juzu ya Nne ya *Al Bidaaya Wan Nihaaya*) na wanahistoria wengine, yeze ndiye aliyekuwa akiwaswalisha wenziwe muda wote wa uamiri wake huo. Kwa hivyo, kama kuswalisha ndiyo hujja yenu, Amru bin al-Aas alikuwa na haki zaidi ya kuwa Khalifa kwa vile ambavyo hata Khalifa wenu wa Kwanza na wa Pili waliwahi kuwa maamuma wake!

Kutokana na hujja yenu hiyo, ingelitaka kila ali- yeteuliwa na Mtume s.a.w.w. kuswalisha awe Khalifa wake. Mbona haikuwa hivyo?

Sababu yetu ya *sabaa* ni kwamba kama kweli Bwana Mtume s.a.w.w. alimuamrisha Abubakar aswalishe watu, na kama hilo humfanya mtu awe Khalifa, munge-likuwa muna *nassi* ya Mtume s.a.w.w. Lakini nyinyi wenyewe masunni mwakataa kuwa Mtume s.a.w.w. aliacha *nassi* ya nani awe Khalifa baada yake!

Sababu yetu ya *nane* ni kwamba, walipokutana baa-dhi ya maswahaba katika ukumbi wa Saqifa kumchagua Khalifa baada ya Mtume s.a.w.w., wale waliopendelea awe Abubakar hawakuitaja hujja hiyo ya kuswalisha! Badali yake walitaja hujja ya “kuwa karibu na Mtume s.a.w.w.” na “Ukureshi”! Kwa nini hiyo ya kuswalisha haikutajwa na yoyote kati ya waliomuunga mkono? Hata na yeze mwenyewe Abubakar!

Sababu yetu ya *tisia* ni kwamba hata yeze mwenyewe Abubakar hakuelewa kuwa kuteuliwa kwake kuswalisha kulikuwa ni alama ya yeze kufanywa Khalifa baada ya Bwana Mtume s.a.w.w. Kama alielewa hivyo, kwa nini hakuitoa hujja hiyo kule Saqifa pale *answaar* waliposimamisha mtu wao? Au kwa nini yeze, pale upinzani ulipokuwa mkali, alipendekeza achaguliwe Umar bin al-Khattaab au Abuu Ubayda bin al-Jarraah badali yake? Kama kuswalisha ni hujja, kama munavyodai nyinyi, huoni hapo kwamba Abubakar alikwenda kinyume

na uamuzi wa Bwana Mtume s.a.w.w. kwa kujitoa yeye na kupendekeza wengine? Jee, ndivyo hivyo?

Mpaka hapa nishakueleza sababu zetu tisia za kukatalia hujja yenu ya kuwa Abubakar ndiye aliyefaa kuwa Khalifa wa Kwanza wa Mtume Muhammad s.a.w.w. kwa sababu alimteuwa kuswalisha watu kabla ya kufariki dunia. Sasa nipe hujja yako ya tatu.

**SUNNI:** Hujja yangu ya tatu, inayotolewa na mashekhe wetu, ni ile ya *ijmaa*; ya kuwa Sayyidna Abubakar alichaguliwa kwa komangano la maswahaba wote.

### HAKUKUWA NA IJMAA (KOMANGANO)

**SHIA:** Hujja hiyo pia tunaikataa... kwa sababu! Na sababu zetu ni hizi:

**Kwanza:** kwa mujibu wa misingi ya sharia ya Kiislamu, *ijmaa* haisimami mbele ya *nassi*. Yaani, neno lolote lililoamuliwa na Mwenyezi Mungu na/au Mtume Wake s.a.w.w. haliwezi kuvunjwa na *ijmaa* (komangano) ya watu *wowote*; wawe ni wanazuoni au hata maswahaba. Kwa kuwa mwanzo wa mdahalo wetu nilikutolea ushahidi wa maneno ya Bwana Mtume s.a.w.w., ya kusema ni nani aongoze Waislamu baada ya yeye kuondoka duniani, hatuwezi kuikubali *ijmaa* inay-

opingana na maneno hayo. Katika maneno ya Bwana Mtume s.a.w.w. hamuna Khalifa Abubakar, wala Umar, wala Uthman.

*Pili ijmaa, kwa ijmaa inayotambulika kisharia, ni lazima iwe ni ya watu wote. Na hiyo ya Abubakar hai-kuwa hivyo. Walikuwako waliokataa kumbai.*

**SUNNI:** Ni nani hao?

**SHIA:** Kabla sijakupa majina yao, kuna mambo fulani muhimu yataka uyajue. Nayo ni haya:

*Kwanza wakati wa uhai wa Mtume Muhammad s.a.w.w., mikutano yote ya Waislamu ilikifanywa msikitini. Kwa nini huo wa kumchagua Khalifa wa Kwanza haukufanywa msikitini; badali yake ulifanywa kwenye ukumbi?*

*Pili waliokuwako kwenye mkutano huo ni *answaar na muhaajiriin* watano tu; si maswahaba wote waliokuwako Madina. Kwa nini hawakukusanyika maswahaba wote, angalau wa Madina peke yake? Na kwa nini *muhaajiriin* wengine wakubwa wakubwa, wakiwamo jamaa zake Mtume s.a.w.w., hawakuwako kwenye mkutano huo?*

**SUNNI:** Tuyaache hayo kwa sasa. Kwanza nitajie hao waliokataa kumbai Abubakar.

**SHIA:** Vyema! Wa kwanza ni Zubayr bin al-Awwaam. Wa pili, Khaalid bin Said. Wa tatu, Mikdaad bin al-As'wad. Wane, Salmaan al-Faarisi. Wa tano, Abuu Dharr al-Ghifaari. Wa sita, Ammaar bin Yaasir. Wa sabaa, Barraa bin Aazib. Wa nane, Ubayy bin Ka'b. Wa tisia, Sa'd bin Abii Waqqaas. Wa kumi, Twalha bin Ubaydillaah. Wa kumi na moja, Utba bin Abii Lahab. Wa kumi na mbili, Far'wa bin Amru. Wa kumi na tatu, Sa'd bin Ubaada.

Hapo sikukutajia jamaa zake Mtume s.a.w.w. (Bantu Haashim), akiwamo Imam Alii a.s., ambao wote walikataa kumbai.

**SUNNI:** Sawa! Lakini hayo yalikuwa kwa muda tu. Baadaye si walimbai? Kwa mfano, yeeye mwenyewe Alii bin Abii Twaalib, halimbai baadaye?

## NGUVU ZILITUMIKA

**SHIA:** Ni kweli, alimbai. Lakini si kwa kхиari. Palitumika nguvu.

**SUNNI:** Palitumika nguvu gani?

**SHIA:** Wanavyotueleza wanahistoria, mambo yalikuwa hivi:

Baada ya Abubakar kuchaguliwa, baadhi ya wale waliokataa kumbai - akiwamo Imam Alii a.s. - waliku-

tana nyumbani kwa Bibi Fatma a.s., binti yake Mtume s.a.w.w. Walipopata khabari hii, Khalifa Abubakar alimtuma Umar bin al-Khattaab na wenziwe wende huko wawatoe ili waje kumbai, na kwamba wakikataa wapigane nao. Umar akatoka na kinga cha moto ili, kama itahitajika, aitie moto nyumba ya Bibi Fatma a.s.! Waandishi wengine wasema aliwahi kamwe kuitia moto! Baada ya hapo, kwa ufupi, ndipo Imam Alii a.s. alipombai Khalifa Abubakar.

Kauli nyengine ni kwamba hakumbai mpaka baada ya Bibi Fatma kufariki dunia. Jee, *bay'ah* ya nguvu kama hiyo utaiita *bay'ah*?

Wala si hao waliokuwako nyumbani kwa Bibi Fatma peke yao waliotumiliwa nguvu. Kuna na swahaba mwengine mkubwa aliyepatwa na kama hayo, kabla ya huo mkasa wa nyumba ya Bibi Fatma a.s.

**SUNNI:** Hilo tuliache kwanza. Nieleze hayo ya nyumba ya Bibi Fatma; yamo katika vitabu gani? Vya mashia?

**SHIA:** Hasha! Yamo katika vitabu vyenu wenyewe, kama:

1. *Ansaabil Ashraaf*, Juzuu ya Kwanza, uk 586 na 587.

2. *Taariikhul Khamiis*, Juzuuy ya Pili, uk 168 na 178.
3. *Taariikhu Abil Fidaa*, Juzuuy ya Kwanza, uk 156.
4. *Al-Iqadul Fariid*, Juzuuy ya Tatu, uk 64.
5. *Muruujudh Dhahab*, Juzuuy ya Pili, uk 100.
6. Diwani ya Haafidh Ibraahiim wa Misri.
7. *Taariikhul Ya'quubii*, Juzuuy ya Pili, uk 126.

**SUNNI:** Na huyo swahaba mkubwa aliyepatwa na kama hayo ni nani?

**SHIA:** Huyo ni Sa'd bin Ubaada.

Bwana huyu ni miongoni mwa viongozi wa *answaar*. Ni katika waliombai Mtume Muhammad s.a.w.w. kule Aqaba, na aliyeshiriki katika vita vyote isipokuwa vile vya Badri ambavyo wanahistoria wanakhitalifiana; wengine wasema alishiriki, wengine wasema la. Pia imepokewa kuwa alikuwa karimu. Yeye alikataa kumbai Abubakar, na hata Umar. Aliuliwa huko Sham katika mwaka wa 15H, baada ya kufumwa mishale miwili iliyosingiziwa majinni!!

Pale maswahaba walipokutana Saqifa, na pakatokea zogo, ilikuwa karibu watu wamkanyage bwana huyu am-

baye alikuwa mgonjwa wakati huo. Watu wake walipoz-indua wale wengine wasimkanyage, Umar bin al-Khatt-waab alisema: "Muuweni! Mwenyezi Mungu amuuwe!" Kisha akamsimamia, akamwambia: "Nilitamani niku-kanyage mpaka nikuvunje viungo vyako!" Hapo Qays bin Sa'd, mtoto wake, akazishika ndevu za Umar, akam-wambia: "Wallwahi, lau ungelimfuchua unywele mmoja tu, usingelirejea na mwanya mdomoni mwako." Ndipo Abubakar alipoingia kati, akamwambia: "Pole pole ewe Umar! Upole hapa ni bora." Umar akaondoka.

Jee, uchaguzi huo ulikuwa ni wa khiari?

Kama wataka kuyaona hayo, tizama uk 455-459 wa Juzuuy ya Tatu ya *Taariikhut Twabarii*.

### **IMAM ALII A.S. HAKUNYAMAZA BALI ALIGOMBA**

**SUNNI:** Lakini kama haki ilikuwa ni yake, mbona Imam Alii hakugomba wala hakuteta?

**SHIA:** Hivyo ndivyo munavyodai nyinyi. Lakini hivyo sivyo. Vilivyo ni kwamba hakunyamaza; aligomba.

**SUNNI:** Kwa ushahidi gani?

**SHIA:** Kwa ushahidi uliomo uk 11-12 wa kitabu cha Ibn Qutayba kiitwacho *Al-Imaamah Was Siyaasah*.

Humo, baada ya kutaja vile Imam Alii alivyochukuliwa na kupelekwa mbele ya Khalifa Abubakar, na kuambiwa ambai Abubakar, alijibu: "Mimi nina haki zaidi ya jambo hili kuliko nyinyi. Sitawabai, hali nyinyi ndio awlaa wa kunibai mimi. Mumelitwaa jambo hili kwa *anshaar*, mukawatolea hujja kwamba nyinyi ni akraba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na sasa mu-naunyakua kwetu *ahlul bayt*. Si mulidai kwa *anshaar* kwamba nyinyi ni awlaa wa jambo hili kwa kuwa Muhammad ametokana na nyinyi? Ndipo walipowapa uwongozi wakatwii amri yenu. Basi na sisi ni awlaa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (kwa vile sisi ni *ahlu bayt* wake) akiwa hai na akiwa maiti. Hebu tuswafieni nyoyo mukiwa mu waumini. Kama sivyo, basi bebeni dhulma (hii) na hali munajua."

Na pale Abuu Ubayda alipomnaswihi amuachie Abubakar kwa kuwa yeye ni mzee mwenye uzoevu am-bao yeye (Imam Alii a.s.) hana, alimjibu: "Tahadharini! Tahadharini! Enyi *muhaajiriin!* Musiutoe utawala wa Muhammad kwa Waarabu kutoka nyumbani kwake na kitovu cha nyumba yake, na kuupeleka majumbani mwenu na vitovu vyta majumba yenu. Wala musiwa-zuiye watu vyeo vyao na haki yao kwa watu. Naapa kwa Mwenyezi Mungu, enyi *muhaajiriin!* Sisi tuna haki zaidi ya makamu haya kwa sababu sisi ni *ahlul*

*bayt.* Na sisi tuna haki zaidi ya jambo hili maadamu miongoni mwetu yuko anayekisoma Kitabu cha Mwenyezi Mungu, anayeielewa dini ya Mwenyezi Mungu, mjuzi wa sunna za Mtume wa Mwenyezi Mungu, bingwa wa mambo ya raia, mwenye kuwakinga na mambo maovu, mwenye kuwagawanyia (haki yao) kwa usawa. Wallahi, miongoni mwetu yuko mtu (kama) huyo. Basi musifuate matamanio, mukaipotea njia ya Mwenyezi Mungu, mukazidi kuwa mbalimbali na haki.”

Hali kadhaalika pale Abubakar alipomtuma huru lake, Qanfad, akamwambia: “Khalifa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu anakwita.” Imam Alii a.s. alimjibu: “Mu wepesi mno wa kumsingizia Mtume wa Mwenyezi Mungu!” Khalifa Abubakar akamtuma tena Qanfad amwambie Imam Alii kuwa “Khalifa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu anamwita akambai.” Alipofika akamwambia hivyo, Imam Alii a.s. aliinua sauti yake, akasema: “*Subhaanallah ! Hakika amedai ambalo si lake.*”

Kwa hivyo, Imam Alii a.s. hakunyamaza.

## **KWA NINI HAKUPIGANA VITA?**

**SUNNI:** Lakini mbona hakupigana na hao waliompokonya haki yake, kama kweli walimpokonya?

**SHIA:** Kuna sababu na hikima ya kufanya hivyo. Na ili uweze kuelewa sababu na hikima hiyo, itabidi uielewe khatari iliyoukabili Uislamu huko Bara Arabu mara tu baada ya Mtume Muhammad s.a.w.w. kufariki dunia.

Utakumbuka kwamba Muhammad s.a.w.w., alipo-tangaza kuwa yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, watu wa kwanza kumpinga walikuwa jamaa zake: watu wa Makka. Wala hawakumpinga kwa maneno tu – yeye na wafuasi wake wachache – bali walipanga hata kumuwa! Ikambidi ahamie Madina ambako alianza ku-pata wafuasi.

Lakini hata huko Madina, alikopata nguvu kuliko Makka, watu wa Makka hawakumuachia. Wakishirikiana na Mayahudi waliokuwako huko, pamoja na wanafiki wengine, walipanga kila njama za kuipinga dola mpya ya Kiislamu aliyoianzisha huko. Waliunda majeshi na wakapigana naye vita kadhaa wa kadhaa. Ni jambo linalojulikana katika historia kwamba, katika vita vyote hivyo, hakuna mtu aliyefaulu kuuwa viongozi na vigogo vya makafiri wa Makka kuliko Imam Alii a.s. - jambo lililomjengea chuki kubwa na upinzani mkali khaswa baada ya Bwana Mtume s.a.w.w. kufariki dunia.

Kwa njama zao kutofua dafu, na kwa kushindwa katika vita vyao dhidi ya Uislamu, watu wa Makka

mwishowe walislimu - wao na viongozi wao waliobakia. Lakini kusilimu kwao hakukuwa ni kwa khiari; kulikuwa ni kwa kukosa budi. Wengi wao walislimu shingo upande, wakingojea wakati ufike wa kulipa kisasi cha hizaya na fedheha iliyowapata.

Fursa hiyo ilipatikana pale mara tu khabari ilipotoka ya Bwana Mtume s.a.w.w. kutawafu. Njama zili-pangwa za kuhakikisha kwamba, kinyume na maagizo ya Mtume Muhammad s.a.w.w., Imam Alii a.s. hatakuwa Khalifa wake wa kwanza, bali hatakuwa Khalifa kamwe!

Mara kukazuka fitina ya wengine kuritadi na kurejea ukafirini, na wengine kadhaa wa kadhaa kujasiri kudai utume kwa kukataa kuwa Muhammad alikuwa Mtume wa Mwisho! Wanafiki, waliotoweka mara tu baada ya Waislamu kuiteka Makka, wakazuka! Ikawa tenge tahanani.

Hayo, kwa ufupi yalikuwa ni ya ndani. Kwa nje, kuona vurugu na udhaifu ulioiingilia dola changa ya Kiislamu, Warumi na Wafursi-dola kubwa za zama hiso - nao walijiandaa kuwashambulia Waislamu.

Katika hali ya khatari na ya kuhuzunisha kama hiyo, Imam Alii a.s. afanyeje? Asimame, akiungwa mkono na wafuasi wake, apigane vita na sirikali ya

Kiislamu inayotawala, japo imempokonya haki yake?  
Au angojee wakati mwengine ulio muwafaka wa kudai  
haki yake hiyo?

Bila shaka, kama wakati huo angeliamua kupigana  
vita vyta kudai haki yake, angelizidi kuidhoofisha siri-  
kali iliyokuwako isiweze kupambana na uadui na up-  
inzani uliojitekeza kwa ndani wala kwa nje – sirikali  
ambayo yeye, kwa kiasi kikubwa sana, alichangia kui-  
simamisha. Kwa hivyo hii ndiyo sababu ya yeye ku-  
topigana vita na hao waliompokonya haki yake, kama  
anavyoeleza yeye mwenyewe.

Kwa mfano, pale alipomteuwa Maalik al-Ashtar  
kuwa Liwali wake wa Misri, Imam Alii a.s. aliwaandikia  
barua watu wa Misri. Katika barua hiyo aliandika:  
“Baada ya yote, Mwenyezi Mungu aliyetakasika al-  
imtuma Muhammad s.a.w.w. kuwa muonyaji kwa vi-  
umbe vyote na msimamizi wa Mitume yote. Alipofariki  
dunia, Waislamu walizozania jambo hili (la Ukhilifa)  
baada yake. Wallahi! Halikuwa likinipitikia moyoni  
mwangu kuwa Waarabu watafazaishwa na jambo hili  
baada yake s.a.w.w., watake kuwapokonya *ahlu bayt*  
wake, wala kwamba watanigeukia. Kwa hivyo haku-  
na lililonitisha kama kuona watu wamemkusanyikia  
fulani wanambai! Hapo nikajizuiya mpaka nilipoona

watu watoka katika Uislamu na kuwalingania wengine waivunje dini ya Muhammad s.a.w.w.! Ndipo nilipoo-gopa kwamba, kama sitaunusuru Uislamu na Wais-lamu, basi nitauna ukifujwfujwa au ukivunjwawunjwa. Hilo, kwangu mimi, litakuwa ni msiba mkubwa zaidi kuliko kuukosa utawala wangu juu yenu ambao ni starehe za siku chache tu zitakazoondoka, vyovyote vitakavyokuwa, kama yaondokavyo mazigazi, au kama yatawanyikavyo mawingu. Nikabaki katika hali hiyo mpaka la batili likaondoka, na dini ikawa salama...”<sup>3</sup>

Na hivyo ndivyo anavyofanya kila mwenye akili na busara: hutanguliza lililo muhimu zaidi kuliko lililo muhimu tu. Na mambo yalivyokuwa siku hizo hayakuachia nafasi ya kupinga kwa upanga wala kwa hujja. Yalitaka subira na kuvuta wakati. Ndipo aliposema tena: “Mtu halaumiwi kwa kuakhirisha (kudai) haki yake. Hulaumiwa kwa kutwaa kisichokuwa chake.”<sup>4</sup> Hivyo alingojea wakati muwafaka ufike. Na ulipofika, kama historia inavyoshuhudia, aliwakumbusha wale waliokuwa wameisahau au wamejisahaulisha haki yake na ya *ahlu bayt* kwa jumla, na akasimama kidete kui-pigania.

**SUNNI:** Kwa leo nimebakwa na suali moja. Nayo ni hii. Hivi munavyoupanga nyinyi uimamu, wa kushikil-

iwa na kizazi cha Mtume s.a.w.w. peke yake, hamuoni kuwa ni sawa na kusimamisha ukoo wa kifalme (*royal family*)?

## **UIMAMU SI UFALME**

**SHIA:** Hasha; si ufalme! Ufalme ni mfumo wa binadamu; uimamu si hivyo. Ni mfumo wa Mwenyezi Mungu. Mtume s.a.w.w., alipoteuwa hawa maimamu 12, hakuwateuwa kwa kichwa chake. Alifanya hivyo kwa amri ya Mwenyezi Mungu (Sura 5:67) na pia, kama Qur’ani Tukufu inavyotueleza (Sura 53:3 - 4), hakuwa akisema maneno kwa matamanio yake, bali yalikuwa ni wahyi. Kwa hivyo Mwenyezi Mungu ndiye Yeye aliywateuwa Mitume aliowatuma (Sura 28:68).

Sasa, tunapoisoma Qur’ani Tukufu (Sura 29:27) tunamuona Mwenyezi Mungu anatueleza kwamba alimpaa Nabii Ibrahimu a.s. mtoto na mjukuu - Is’haaq na Ya’kub - na akaweka “utume katika kizazi chake.”

Hali kadhaalika (Sura 57:26) alimpeleka Nuhu na Ibrahimu, na akaweka “utume katika kizazi chao”. Na (Sura 6:84-86) kabla ya kumleta Nabii Ibrahimu, Mwenyezi Mungu alimleta Nabii Nuhu ambaye, “katika kizazi chake”, alitoa mitume kadhaa wa kadhaa: Daudi, Suleimani, Ayubu, Yusuf, Musa, Harun, Zakariya,

Yahya, Isa, Ilyaa, Ismaaiil, Ilyasa', Yunus, Lut.

Kama ni hivyo basi, viyi itakuwa mfumo wa maimamu kutoka *katika kizazi cha Mtume* ni mfumo wa ukoo wa kifalme, ule wa Mwenyezi Mungu wa kutoa Mitume *katika kizazi cha Nabii Nuhu* usiwe hivyo, hali mifumo yote miwili imewekwa na huyo huyo Mwenyezi Mungu mmoja? Lizingatie hilo kwa makini.

Naomba kwa leo tukomee hapa. Tungojee kikao chengine tutakapolumbana ya Imam Mahdi a.f. ('*ajjalallaahu farajah*).

## VIDOKEZO

1. Kwa Kiarabu ni *Kitaabus Swalaaah*, Mlango wa *Man Qaama Ilaa Jambil Imaami Li'illah* na *Ar Rajuli Ya'tammu Bil Imaami Waya'tammun Naasu*
2. *Bil Ma'mumi*.
3. Kwa Kiarabu ni Mlango wa *Kitaabun Nabiyyi s.a.w.w. Ilaa Kisraa wa Qayswara*.
4. Barua Na. 62 katika *Nahjul Balaagha*.
5. Maneno ya hikima Na. 166 ya Imam Alii a.s. katika *Nahjul Balaagha*.

## VITABU VYENGINE VYA SHEIKH ABDILAH NASSIR:

1. Al-Battaar: Sherehe ya Dhul Faqaar
2. Tafsiri ya Sura At-Talaq
3. Tafsiri ya Juzuuy 'Amma
4. Shia na Qur'ani
5. Shia na Sahaba
6. Shia na Hadith
7. Maulidi: si bid'a si haramu
8. Ukweli wa Hadith ya Karatasi
9. Mut'a: Ndoa ya Halali
10. Shia na Taqiya
11. Yazid Hakuwa Amiirul mu'minin
12. Yazid Was Never Amiirul mu'minin
13. Malumbano Bainay Sunni na Shia (ni hiki)
14. Sura Al-Ahzaab: Tafsiri na Maelezo (Kinata-yarishwa)

---

## **ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION:**

---

1. i) Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili  
ii) Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuuy ya kwanza  
mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (a.s.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swalaa
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudhar
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu

21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamilii wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua kwa Mujibu wa Ahlulbayt (a.s)
33. Udhuu kwa Mtazamo wa Qur'ani na Sunna
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Qur'ani na Kuhifadhiwa Kwake
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya Sala Mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipyta

46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an Yatoa Changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina - 'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuuy ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuuy ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini

71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam ‘Ali na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-lлаah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Dhana ya Ndoa ya Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raj’ah)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni Na Njiani
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali (AT- TAWASSUL)
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia

96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenyе kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Maimamu wa Ahlul Bait – Ujumbe na Jihadi
100. Idi Al-Ghadir
101. Kusoma sura zenyе Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunna za Nabii Muhammad (saww)
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Mwanamke Na Sharia
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqaalain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano

121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifua Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vy'a kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vy'a kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)  
(Sehemu ya Kwanza)
131. mam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)  
(Sehemu ya Pili)
132. Khairul l'Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. Adhana ni Ndoto au ni Wahyi?
136. Tabaruku
137. Saada Kamili – Kitabu cha Kiada cha Maadili
138. Vikao vy'a furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vy'a wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mjadala wa Kiitikadi

145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt  
(Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Shia na Qur'ani – Majibu na Maelezo
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka

170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. as-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhan)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Historia maana na lengo la Usalafi
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa

195. Upotoshaji Dhahiri katika (Turathi) Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina (as) na Makhalifa
197. Tawheed Na Shirki
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa Abu Bakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni waKisunni na Kishia (Al- Muraja'aat)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebisho na Mageuzi
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza
213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo

219. Maeneo ya Umma na Mali Zake
220. Nahju ‘L-Balagha– Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
222. Mazingatio Katika Swala
223. Imam Hasan na Mfumo wa Kujenga Jamii
224. Vyakula Na Vinywaji
225. Kuelewa Rehema ya Mwenyezi Mungu
226. Imam Mahdi na Bishara ya Matumaini
227. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
228. Shia Na Sahaba - Majibu na Maelezo
229. Majanga Na Jukumu la Jamii
230. Shia Na Hadith - Majibu na Maelezo
231. Upotofu Ndani ya Kitabu cha Mitaala kwa Shule za Sekondari
232. Ugaidi Wa Kifikra Katika Medani Ya Kidini
233. Yafaayo kijamii
234. Uswalihina Dhahiri Na Batini Yake
235. Mkakati wa Kupambana na Ufakiri
236. Mwanamke Katika Harakati Za Mageuzi
237. Jihadi
238. Hija Katika Maneno Na Ujumbe Wa Imam Khomeini (R.A)
239. Tiba Ya Maradhi Ya Kimaadili
240. Yusuf Mkweli

241. Taqiyya Kwa Mujibu Wa Sheria Ya KIISLAMU
242. Imam Mahdi (A.S) Imam Wa Zama Hizi Na Kiongozi Wa Dunia
243. Talaka Tatu
244. Safari Ya Kuelekea Kwa Mwenyezi Mungu
245. Hotuba Za Kiislamu Juu Ya Haki Za Binadamu
246. Mashairi Ya Kijamii
247. Ngano Ya Kwamba Qur'ani Imebadilishwa
248. Wito Kwa Waumini: "Enyi Mlioamini"
249. Imam Husain (a.s) ni Utu na Kadhiya
250. Imam Husain ni Kielelezo cha Kujitao Muhanga na Fidia
251. Imam Mahdi ni Tumaini la Mataifa
252. Kuchagua Mchumba
253. Mazungumzo ya Umoja – Ukossoaji na Usahihishajji
254. Utamaduni wa Mwamko wa Kijamii
255. Hekima za kina za Swala
256. Kanuni za Sharia za Kiislamu
257. Utamaduni kufuatana na Qur'ani na Utekelezaji wa Kivitendo  
(Sehemu ya Kwanza)
258. Kauli sahihi zaidi katika kufafanua Hadithi

## **KOPI ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA**

---

1. Amateka Na Aba' Khalifa
  2. Nyuma yaho naje kuyoboka
  3. Amavu n;amavuko by;ubushiya
  4. Shiya na Hadithi
  5. Kor'ani Nziranenge
  6. Kwigisha Mu Buryo Bw'incamake Uka Salat Icotwa
  7. Iduwa ya Kumayili
- 

## **ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION KWA LUGHA YA KIFARANSA**

---

1. Livre Islamique